

Historia

Ilipobuniwa wakati wa Vita vya Pili vya Dunia huko Bretton Woods, New Hampshire, Benki ya Dunia mwanzoni ilisaidia kuijenga upya Ulaya baada ya vita. Mkopo wake wa kwanza wa \$250 milioni ulikuwa kwa Ufaransa katika mwaka wa 1947 kwa madhumuni ya marekebisho ya baada ya vita. Marekebisho yameendelea kuwa sehemu muhimu zaidi ya kazi za Benki kwa kushughulikia na mikasa ya hali ya anga, kuangalia pamoja na mahitaji ya kurudisha usawa baada ya vita-shida ambazo zinazikumba nchi zenye chumi changa na zenye kuendelea kukua.

Hata hivyo, Benki ya wakati wa sasa imeimarisha mwelekeo wake kuhusu kuupunguza umasikini na kuufanya kuwa shabaha ya juu zaidi ya kazi zake zote. Kitambo, Benki ilikuwa na wahandisi na wataalamu wa mambo ya fedha ambao shughuli na makazi yao yalikuwa Washington, D.C. Hivi leo, Benki ina wafanyikazi wa tabaka aina mbalimbali na wenye ujuzi wenye upana mkubwa. Kati yao ni: wataalamu wa uchumi, wataalamu wa usimamizi wa sera, wataalamu wa sekta, na wanasayansi wa mambo ya jamii. Asilimia 40 ya wafanyikazi sasa wako katika ofisi za nchi.

Benki yenyewe imezidi kwa ukubwa na upana. Imekuwa Group [Mshikano], unaojumuisha mashirika matano ya maendeleo yaliyo na uhusiano wa karibu zaidi nayo ni: [International Bank for Reconstruction and Development](#) (IBRD) [Benki ya Kimataifa ya Marekebisho na Maendeleo], [International Development Association](#) (IDA) [Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo], [International Finance Corporation](#) (IFC) [Muungano wa Kimataifa wa Fedha], [Multilateral Investment Guarantee Agency](#) (MIGA) [Shirika la Uthibiti wa Uwekezaji], na [International Centre for Settlement of Investment Disputes](#) (ICSID) [Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Mizozo ya Uwekezaji].

Ukiuaji

Katika miaka ya 1980, Benki ilikabiliwa na misukosuko kadhaa: mapema katika mwongo, Benki ilikabiliwa na maswala ya uchumi na mipangilio mipya ya malipo ya mkopo; na baadaye katika mwongo kulikuwa na maswala ya jamii na mazingira, ambayo yalikuwa ya umuhimu mkubwa zaidi, pamoja na shutumu za kuongezeka kutoka kwa watumishi wa umma ambao waliilaumu Benki kwa kukiuka sheria zake zenyewe kuhusiana na miradi yenye umuhimu mkubwa.

Ili iweze kuangalia maswala kuhusu usawa wa shughuli za Benki, Repoti ya Wapenhans ulitolewa na baada ya mda mfupi hatua za marekebisho zilichukuliwa. Hii ilikuwa ni pamoja na kubuniwa kwa Inspection Panel [Kikao cha Ukaguzi] cha kuchunguza madai dhidi ya Benki. Hata hivyo, shutuma iliendelea kuongezeka na ilifikia kikomo katika mwaka wa 1994 wakati wa Mikutano ya Mwaka huko Madrid.

Mabadiliko na Uthabiti

Tangu wakati huo, Mshikano wa Benki umepiga hatua kubwa. Mashirika yote matano yamekuwa yakifanya kazi kibinafsi na kwa pamoja ilikuboresha ufanisi wa ndani na ubora wa nje. Wateja wameonyesha kuridhika kwingi na mabadiliko wanayoyaona katika huduma, moyo wa kujitolea, na kupeana huduma za Mshikano wa Benki.

Zaidi ya ilivyokuwa hapo awali, Benki imekuwa na jukumu muhimu zaidi katika sera za ulimwengu. Imeshirikiana vilivyo pamoja na washirika na wateja wakati wa dharura kuu kama zile za shughuli za baada ya vita vya Bosnia, misaada ya Afrika Mashariki, kazi ya urekebishaji na kuweka sawa baada ya kimbunga katika Amerika ya Kati, na hata katika

kupeana misaada baada ya mitetemeko ya ardhi huko Uturuki, Kosovo na Timor Mashariki.

Mbali na hatua hizi za kuvutia, ajenda ya Mshikano wa Benki bado haija kamilika na itakuwa vigumu kukamilisha bado kukiwa na ongezeko la changamoto za maendeleo.

Ilikupata mwongozo wa matukio ya historia ya Benki, anagalia [Mwongozo wa Matukio ya Historia ya Mshikamano wa Benki](#)

Ujumbe wa Norway,
Bretton Woods,
Julai 1944

Waziri wa Hazina wa Marekani,
Henry Morgenthau, Bretton Woods,
Julai 1944

Mama na binti, Uchina, 1993